| HOT &TOR – Kiswahili B<br>**T106**<br>Wednesday, 28/11/2018<br>02:00 – 05:00 PM |
|---|

WORKFORCE DEVELOPMENT AUTHORITY

WDA

P.O. BOX 2707 Kigali, Rwanda Tel: (+250) 255113365

# Mtihani wa Taifa 2018

**SOMO: KISWAHILI B**

**MICHEPUO: HOTELI (HOT) NA UTALII (TOR)**

**MUDA: MASAA 3**

**MAELEZO:**

- *Mtihani huu ambao una sehemu tatu **I, II** na **III**, una maswali 23 lakini utajibu maswali 19 tu kwa alama 100.*
- *Sehemu ya **I** ina maswali 15 ambapo unapashwa kuyajibu yote kwa alama 55.*
- *Sehemu ya **II** ina maswali 5 amabapo utajibu maswali 3 tu kwa alama 30.*
- *Sehemu ya **III** ina maswali 3 ambapo utajibu swali moja tu kwa alama 15.*
- *Andika vizuri nambari ya kila swali unalolijibu.*
- *Mwandiko wako usomeke na ujiepushe na uchafu.*
- *Tumia kalamu ya bluu au nyeusi.*

**Mtoto na Mbwa mwitu**

Mtoto mmoja alikuwa anarudi peke yake kutoka machungani wakati wa jioni. Alipita katikati ya kichaka ambako alikutana na Mbwa mwitu. Kumbe yule Mbwa mwitu alikuwa na njaa na alijua kuwa mtoto kama yule angetosha kabisa kwa chakula cha jioni kwake na kwa familia yake ya watoto wanne kule pangoni. Alianza kumnyemelea akimmezea mate kwa uchu.

Yule mtoto aliogopa sana, mwili mzima ulitetema, ingawa alijitia ujasiri na hakutaka kufa kikondoo. Alifahamu kuwa hawezi kupambana naye kwa mabavu akamshinda, wala asingeliweza kushindana naye kwa mbio akamzidi. Hivyo alipoona kwamba hakuwa na namna ya kujiepusha na hatari ile, alimgeukia Mbwa mwitu na kumwambia kwa unyenyekevu: "Najua, ee rafiki yangu Mbwa mwitu, kwamba una njaa na mimi ni windo lako, na kwa kuwa sina uwezo wowote wa kujiokoa dhidi yako. Basi kabla ya kuniua, nakuomba unisaidie kitu kimoja tu. Ninakuomba uniimbie wimbo mmoja niupendao ili nicheze kwa mara ya mwisho, kisha nikimaliza uniue na kunila."

Mbwa mwitu aliangua kicheko kusikia ombi la mtoto ambaye kwake alikuwa tayari ni marehemu mtarajiwa. Baadaye alikubali, akachukua filimbi na kuanza kumpigia wimbo.Wakati mtoto anacheza huku akiwa amejawa na hofu, Mbwa wa nyumbani kwake walisikia sauti ile, wakakimbilia pale kabla ya ule wimbo kwisha na kuanza kumtimua yule Mbwa mwitu. Mbwa mwitu alimgeukia mtoto akasema, "Hii ni halali yangu; kwani mimi ambaye wasifu wangu ni muuaji na mla nyama, sikupaswa kugeuka mpiga filimbi ili kukidhi matakwa yako wewe."

Mtoto alirudi nyumbani kwa usalama akisindikizwa na Mbwa wa nyumbani. Alipofika nyumbani, alikuwa akingali na hofu. Wazazi wake walimuuliza kwa nini alikuwa na hofu na ye akawasimulia kwa makini shida aliyopata kutokana na Mbwa wa mwitu aliyekaribia kumla akaokolewa na wale Mbwa wa nyumbani. Wazazi waliposikia hivyo walikuwa na hisia za hofu na furaha. Wale Mbwa wa nyumbani walipewa shukrani na wakachinjiwa kuku.

Tangu siku hiyo, mtoto aliamuwa kutotembea jioni yeye pekee bila kusindikizwa na wale Mbwa wa nyumbani. Alikuwa akisema huwenda angelikutana tena na yule Mbwa wa mwitu akaweza kujilipizia kisasi na kumla.

Yule Mbwa wa mwitu aliporudi pangoni mwake alikuwa na haya kwani alipoondoka alikuwa ameahidi kuwaletea watoto wake chakula, lakini alipata

mkosi. Usiku huo yeye na watoto wake hawakupata usingizi kutokana na njaa amabayo ilikuwa inawauma. Aliamka mapema kuwatafutia chakula. Aliwahi kumkamata sungura na kumletea watoto wake. Hawa walifurahi sana.

## SEHEMU I: UFAHAMU NA MATUMIZI YA LUGHA — ALAMA 55

**Jibu maswali yote katika sehemu hii**

**01.** Je, mtoto huyu alipokutana na Mbwa mwitu alikuwa anatoka wapi? **Alama 3**

**02.** Mbwa mwitu na watoto wake walikuwa wanaishi wapi? **Alama 3**

**03.** Mbwa mwitu alipokutana na mtoto alikuwa katika hali gani? **Alama 3**

**04.** Ni kwa nini Mbwa mwitu alipomwona mtoto alifurahi sana? **Alama 4**

**05.** Mtoto alipokutana na Mbwa mwitu alikuwa na hisia gani? **Alama 4**

**06.** Kitu gani kinachoonyesha kwamba mtoto anamwogopa sana Mbwa mwitu? **Alama 4**

**07.** Mtoto alimuomba Mbwa mwitu nini? **Alama 4**

**08.** Ni nani aliyemuokoa yule mtoto? **Alama 3**

**09.** Onyesha jinsi Mbwa mwitu alikuwa mjinga. **Alama 4**

**10.** Toa vitenzi vitokanavyo na maneno yafuatayo. **Alama 4**

a. Ahadi : b. windo:

**11.** Ni kwa nini Mbwa mwitu na watoto wake walikosa usingizi? **Alama 3**

**12.** Mtoto alichukua uamuzi gani baada ya ile shida? **Alama 4**

**13.** "Mtoto hakutaka kufa kikondoo" eleza maana ya nahau hii. **Alama 4**

**14.** Ni kwa sababu gani wazazi wa mtoto waliposikia yaliyomfikia mtoto wao walikuwa na hisia za hofu na furaha? **Alama 4**

**15.** **"Giza likizidi, kucha kunakaribia"** Fafanua methali hii ukiilinganisha na hadithi ya mtoto na Mbwa mwitu. Inatufundisha nini? **Alama 4**

## SEHEMU II: SARUFI — ALAMA 30

**Jibu maswali matatu tu katika sehemu hii**

**16.** Andika nomino mwafaka kutoka mabano kukamilisha sentensi zifuatazo. **Alama 10**

a. ----- ----- (maji, majembe ) yatachotwa na nani?

b. ------ ------- (nyumba, mlango) utafungwa.

c. ------- -------(karatasi, nyoka) inaanguka chini.

d. Ninaona ----- -------(dirisha, kiti) cha kukalia.

e. Tizama ------ -------(ukuta, habari) mzuri.

**17.** Sahihisha sentensi hizi kama kuna makosa. **Alama 10**

a. Mimi hupenda maziwa ya ngombe.

b. Baada ya kununua tiketi nilimkamata basi.

c. Ninapoandika ninatumia karamu ya bluu.

d. Alijenga nyumba nkubwa.

e. Kama una njaa nitakuuzia chakula.

**18.** Tumia "amba" katika sentensi zifuatazo. **Alama 10**

a. Mwanafunzi ...... ....... husoma kwa bidii hufualu katika mtihani.

b. Ukuta ........ ........... ulibomoka jana ulijengwa tena.

c. Kitabu ..... ......... husomwa sana huraruka.

d. Miti ....... .......ilipandwa imestawi

e. Jisho ....... ......lilitibiwa linaona vizuri

**19.** Tia katika hali yakinishi tungo zifuatazo. **Alama 10**

a. Sijala chakula kizuri.

b. Hatukumuona mwanafunzi huyo .

c. Yeye hapendi ugali.

d. Usingeliniona usingelikuja.

e. Hatutakusubiri.

**20.** Toa kinyume cha vitenzi vilivyopigiwa mstari (usibadili mzizi). **Alama 10**

a. Alifunga mlango.

b. Umevaa kofia uliyonunua sokoni.

c. Zibua tundu linalopitisha maji.

d. Alishona nguo yake.

## SEHEMU YA III: UTUNGAJI — ALAMA 15

**Jibu swali moja tu katika sehemu hii**

**21.** Fupisha hadithi hii katika mistari isiyozidi kumi. **Alama 15**

**22.** Andika hadithi simulizi unayojua. Tumia maneno kati ya 80 na 100. **Alama 15**

**23.** Katika maneno kati ya 80 na 100 eleza shida uliyopata maishani mwako. **Alama 15**